



Kumeme
Na Pendo
Mifugo
Ndaki
ACI Salan
Hembeba
Macharere
Uviji, vijji
ya baadhi
tarehe
D
Uzalishaji
Na Pendo
Ndaki, Hembeba
Tarehe
Macharere
Uviji
Vijji
Na Pendo
Ndaki
PICHA:
TUMAINI
MAPIE

Waziri aonya wanaochochea migogoro wakulima, wafugaji

Na Elizabeth Zaya

WAZIRI wa Mifugo na Uviji, Mashumba Ndaki, amewaonya baadhi ya viongozi wa vijji na kata wanaoshirikiana na wafugaji kuunja sheria kwa kuwanyanya sa wakulima katika maeneo yao.

Ndaki alisema baadhi ya viongozi wa vijji badala ya kuwa watatuza wa migogoro wamegeuka kuwa wachochezi na kusahabisha iendelee wakitafuta maslahi yao binafsi kutoka kwa makundi hayo.

Alisema viongozi wa vijji watakobainika kushiriki katika kuchochaea migogoro hiyo, wataadhibiwa.

Alisema serikali haiko tayari kuvumilia viongozi wanaotengeneza migogoro katikati ya jamii, ili wao wanufaikie na kuwa cha wananchi wakulima.

"Siku zote wakulima na wafugaji wamekuwa ni jamii zinazolewana kwa sababu kila mmoja amekuwa akihitaji huduma kutoka kwa mwenzake, kwa maana ya mazao ya kilimo na mifugo, lakini inapotokea tena eti baadhi ya viongozi wa vijji wanaingiza chuki kati yao na kuwachonganisha kwa maslahi binafsi, hili ni tatizo na ni hatari na sisi hatuwezi kuvumilia haya," alisema Ndaki.

"Serikali haitaangalia nani ni

mpole na nani mkaalii, kundi lolote ambalo tutalibaini kwamba ndilo chanzo cha migogoro tutalidhibu, tunataka kila mru afuate au kuendesha shughuli zake kwa kufuata sheria za nchi na si vinginevyo na tukifanya hivyo itatusaidia kuishi pamoja kwa upendo."

Aliwataka wafugaji kushirikiana na serikali kujenga miundombinu ya ufugaji yakiwamo malambo ya maji ya kunywesheya mifugo yao hususani katika maeneo ambayo wamekabidhiwa na serikali kufuga.

"Mahitaji ya wafugaji ni mengi, wanahitaji malambo, malisho, majosho na minada katika mae-

neo yao wanayofugia, kwa hiyo ni vyema tukishirikiana," alisema Ndaki.

Alisema katika hajeti ijayo, wizara hiyo ina mpango wa kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kujenga malambo katika maeneo mbalimbali nehini kuanzia katika baadhi ya vijji kwa kushirikiana na halmashauri.

"Tunataka kuizalikisha sektaa hii inakuwa chache ya maendeleo katika nchi yetu, tunahakikisha kwamba tunarweka miundombinu mizuri ambayo itasaidia kufikia katika malengo makabowa ya uzalishaji tunayoyataka katika nchi yetu," alisema Ndaki.

Mwisho

'Mifugo ipatiwe chanjo mapema'

Aurea Simtowe, Mwananchi
asimtowe@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Wakati ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha chanjo nchini kikitarajia kukamilika Aprili 2021 wafugaji wameagizwa kuptatia chanjo mifugo yao ili iweze kuondokana na magonjwa.

Licha ya kiwanda hicho cha Hester kilichopo Kibaha kukaribia kukamilika, imebainishwa kuwa Tanzania ina chanjo za kutosha kudhibiti magonjwa ya mifugo.

Akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Pwani, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema kukamilika kwa kiwanda hicho kutasaidia kuongeza wigo wa uwepo wa chanjo nchini.

Kuhusu wafugaji kuipatia mifugo yao chanjo, alisema jambo hilo litasaidia upatikanaji wa mazao bora ya mifugo.

"Tunazo chanjo za kutosha, hivyo niwatake wafugaji wote ikiwa ni pamoja na sisi Serikali kwenye maeneo tunayofuga tuchanje mifugo yetu ili tupate mifugo bora," alisema Ndaki.

"Tunataka sasa nchi yetu iende kwenye ubora badala ya uwingi wa mifugo, ili tupate nyama bora na maziwa bora kwa maana ya mazao bora ya mifugo ili tuweze kuuza katika soko la kimataifa."

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo alisema migogoro ya wakulima na wafugaji imepungua kwa kiasi kikubwa huku akitaka juhudzi zaidi zifanyike katika kuwapatia wafugaji elimu ya kuwa na mifugo michache na yenye tija.

Nuisance taxes cripple meat exports - traders

From DAILY NEWS
Reporter in Longido

An appeal has been made to the government to consider reviewing some nuisance taxes and levies which hinder investors in livestock industry.

The taxes, they said, impede the investors from competing in the international market, especially in exporting meat and other livestock products to neighbouring countries.

Such an appeal was made by the Director of Eliya Food Overseas Ltd, Shabbir Virjee to the Deputy Minister of Livestock and Fisheries, Ms Pauline Gekul who visited the factory's operations at Namanga Border Village recently.

Mr Virjee said neighbouring counterparts in Ethiopia, Kenya, Somalia and Uganda sell their livestock at much lower prices due to minimal taxes and levies.

"The biggest challenges we face is taxes and levies...currently, we are paying at least five taxes before exporting our

livestock products, this has made it difficult for us to compete in the international market because our products sell at much higher prices," said Mr Virjee.

He identified some of the nuisance taxes and levies to include 50/- paid to the Ministry of Agriculture for a kilogramme, the Meat Board secures a percentage of the total value, the Muslim Council of Tanzania (Bakwata) for Halal license, while 0.1 per cent is paid for radiation taxes among other licenses.

He added that "They usually pay the taxes at each and every step, something which is hindering them from thriving and competing with their neighbours who charge less".

Besides, another challenge facing the investors is lack of enough livestock as raw materials in the factory, calling on the government to intervene so that they can get more livestock for processing.

The Director noted that most of the herders sell their livestock in Kenya because the price there is appealing.

They requested the deputy minister to assist them to acquire reliable raw materials for their factory, citing that the factory slaughters only 2000 goats and 400 cattle daily, which is less than the actual demand.

According to him, if the current situation continues, running the factory will become difficult, taking into account that they will fail to meet both the inside and outside market.

He disclosed that the bigger goal of the factory was to create jobs for more than 150 Tanzanians. Ms Gekul applauded the investors for the efforts they have put in establishing the industry and fulfilling President John Magufuli's aspiration of industrialising the country, pledging to work on the highlighted challenges.

She directed the Permanent Secretary of the responsible ministry, Prof Elisante Ole Gabriel to formulate a team to follow up on the highlighted issues, including the one relating to herders sending their livestock to neighbouring countries.

**DEPUTY
Minister for
Livestock
and Fisheries
Pauline Gekul
(right) and
Director of
Fisheries
Development
Division
Magese Bulayi
look at a fish
variety when
she toured XIN
SI LU fish farm-
ing company
in Manyara
Region
recently.
(Photo by Staff
Photographer)**



Serikali kuvalia njuga soko la nyama kimataifa

Na MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali itafanya mawasiliano na Wilaya za Mambo ya Nie za mafuraha moalimbalii ambayo basidhi ya viwanda vya Tanzania vinapata changamoto ya vibali vya kusafirisha nyama iliyochakatwa.

Akizungumza katika ziara yake ya siku mbili mkoani Pwani Ndaki, alisema mawasiliano hayo yanafanyika pia kwa Wilaya za Viwanda na Biashara za nchi hizi.

Alisema shabaha ya mawasiliano ni kufahamu changamoto zinazovikabili baadhi ya viwanda nchini, kushindwa kusafinsha nyama kwenda baadhi ya nchi na kukosa vibali vya kuingiza nyama hizo kutoka Tanzania.

Hata hiyo, Ndaki, alisema uwepo wa viwanda vya kuchinjia na kuchakata nyama unasaidia kubadilisha fikra za wafugaji na kujikita kwenye ufugaji wenye tiba.

Pia utasaidia kukuza biashara ya mifugo na kutanua wigo wa masoko, hiyo wafugaji na tajifa

kuwanufaisha,

Ndaki alisema atahakikisha uwepo wa chanjo za kutosha dhidi ya magonjwa ya mifugo, hivyo wafugaji wanapaswa kuchanja mifugo ili kuepuka magonjwa.

"Tunazo chanjo za kutosha wafugaji wote ikiwa ni parmoja na sisi serikali kwenye maeneo ambayo tunafuga tuchanje mifugo yetu ili tupate mifugo bora, tunataka sasa nchi yetu iende kwenye ubora badala ya wingi wa mifugo".

Allongeza, "ili tupate nyama bora na maziwa bora kwa

maana ya mazao bora ya mifugo na kuvuna soko la kimataifa ni budi tuzingatie chanjo ya mifugo yetu".

Alisema atasimama vyema kukabiliana na kero za wilaya hiyo na atahakikisha zinazafanyiwa kazi ili kulnua sekta ya mifugo na kuondoa migogoro isiyi na tija.

Pia, alitaka wafugaji wa Rufiji kuhestimu maeneo walijopewa na uongozi wa mkoa kwa ajili ya ufugaji na kuacha kuingia katika maeneo ya wakulima.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) Dk. Stella Bitanyi,

alisema chanjo zimesambawia kutokana na muhitaji ya ranchi mbalimbali na wilpo katika hatua ya kuwafikia majirani ili kuchanja ng'ombe wao.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhandisi Everett Ndikilo, alisema migogoro ya wakulima na wafugaji imepungua kwa kiasi kikubwa huku alitaka juhud zaidi zilanyike katika kuwapatia wafugaji elimu ya kuwa na mifugo michache na yenye tija badala ya kuwa na mifugo mingi ambayo halioshi kutokana na uwepo wa maeneo ya kuifugia.